**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB) KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA MAAFISA HABARI NA UHUSIANO WA SERIKALI, UKUMBI WA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA (MUST), MBEYA TAREHE 24 MEI, 2021.**

- **Mhe. Juma Homera, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya;**
- **Mhe. Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**
- **Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**
- **Profesa Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI;**
- **Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**
- **Ndugu Gerson Msigwa, Mkurugenzi, Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali;**
- **Ndugu Paschal Shelutete, Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari na Uhusiano Serikalini (TAGCO);**
- **Watendaji Waandamizi wa Serikali ambao wako nasi hapa;**

- **Maafisa Habari Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania............. Kazi Iendelee.**

Asalam Aleikum;

Bwana Yesu Asifiwe;

Tumsifu Yesu Kristu.

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika salama hapa Jijini Mbeya kutoka mikoa mbalimbali nchini. Ni matumaini yangu kuwa kila mtu ameamka akiwa mwenye afya njema na yupo tayari kushiriki kikamilifu katika kikao hiki muhimu. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru waandaaji wa Kikao hiki wakiongozwa na Katibu Mkuu wangu, Dkt. Hassan Abbasi kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Idara ya Habari – *MAELEZO* na Msemaji Mkuu wa Serikali, Bw. Gerson Msingwa, timu nzima ya Idara ya Habari pamoja na Viongozi wa TAGCO wakiongozwa na Mwenyekiti Bw. Pachal Shelutete.

Napenda pia kuzipongeza Wizara, Taasisi za Umma na Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji ambazo zimeitikia wito wa kuja kushiriki kikao hiki. Kipekee niwashuiuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, **Mheshimiwa Juma Homera** kwanza kwa kuendelea kuaminiwa na Mhe. Rais na kukuhamishia Jiji la Mbeya ili kuendela kuwatumikia wananchi. Aidha, nikupongeze pia kwa kukubali kuungana nasi kwenye ufunguzi wa kikao hiki ikizingatiwa kuwa kinafanyika katika Mkoa wako, na nimshukuru pia Mkuu wa Chuo cha Sayansi na Technolojia Mbeya, kwa upendo aliounesha kwa Maafisa Habari na kuruhusu Kikao Kazi hiki kufanyika hapa Chuoni kwake, tena bila kulipia gharama zozote. **Kwa pamoja niwashukuru sana.**

**Ndugu Washiriki**;

Nimefurahi kupata fursa hii adhimu ya kufungua kikao hiki muhimu kwa mwaka huu 2021 ikiwa ni mara yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ikumbukwe kwamba, kikao hiki ilikuwa kifanyike mwezi Machi, lakini kama mnavyofahamu kiliahirishwa kutokana na msiba mkubwa uliopata Taifa letu kwa

kuondokewa na Rais wetu Mpendwa, Hayati, Dkt. John Pombe Magufuli. Naomba tusimame kwa dakika moja kumkumbuka Jemadari huyu.

**Ndugu Washiriki;**

Kikao kazi cha mwaka huu kimekuwa na umuhimu wake hatika historia ya nchi yetu kwa kuwa ni cha kwanza katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini Rais wetu **Mhe. Samia Suluhu Hasan**. Tunatambua kuwa, tangu achaguliwe kuwa Rais, amekuwa akisisitiza juu ya uwajibikaji wa kila mtu katika nafasi yake. Aidha, kauli mbiu yake ya "***Kazi Iendelee***" inatilia mkazo juu ya wajibu wa kila mtu katika kutekeleza majukumu yake.

**Ndugu Washiriki**;

Nimeguswa na Kauli Mbiu ya kikao cha mwaka huu isemayo: "***Utoaji Taarifa kwa Umma ni Takwa la Kisheria, Viongozi wa Umma na Maafisa Habari Tuwajibike***." Kauli mbiu hii inasisitiza juu ya umuhimu wa kikao hiki ambacho kitakuwa na mada kadhaa zitakazowasilishwa kwa siku tano mtakazokuwa hapa. Nimeelezwa kuwa, miongoni mwa mada zitakazowasilishwa ni namna mnavyopaswa kuboresha utendaji wenu wa kazi ili kuongeza weledi na mikakati ya namna bora ya kuimarisha mawasiliano Serikalini ikiwa ni pamoja na kuisemea Serikali katika nafasi zenu. Aidha, nimeelezwa kuwa, pamoja na mada zitakazowasilishwa, mtajifanyia tathmini ya utekelezaji wa majukumu yenu kwa mwaka 2021 ili kutekeleza kauli ya Baba wa Taifa inayosema **"*Kujikosoa ni Kujisahihisha.*"**

**Ndugu Washiriki;**

Moja ya mambo ambayo Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa sasa tunayafanyia kazi ni mageuzi makubwa katika kusimamia utoaji wa huduma za habari kwa umma. Mtakumbuka kwamba, Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha sheria mbili, moja ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na Sheria ya Haki ya Kupata Habari ya Mwaka 2016.

Lengo la msingi la Sheria ya Huduma za Habari ni kusaidia watu kupata habari; kueleza aina ya taarifa ambazo jamii ina haki ya kuzipata; na kusisitiza uwazi na uwajibikaji kwa vyombo au watu wenye taarifa. Sheria ya Haki ya Kupata Habari inalenga kusaidia watu kupata taarifa; kueleza aina ya taarifa ambazo jamii ina haki ya kuzipata; na kusisitiza uwazi na uwajibikaji kwa vyombo au watu wenye taarifa. Katika kutekeleza sheria hizi, tunaamini kwa dhati kuwa wananchi sasa watapata taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali na mafanikio yake na wao kutoa maoni yao kuhusu taarifa wanazopata na pia kupata taarifa hizo.

**Ndugu Washiriki;**

Wakati tunakutana hapa Mbeya, Serikali tayari imeshachukua hatua mbalimbali za kuimarisha Sekta ya Habari kupitia sheria hizi. Utekelezaji wa Sheria hizi umeanza kwa viwango tofauti na muda mfupi ujao tunatarajia kuanzishwa kwa vyombo kama vile Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la Habari. Bodi ya Ithibati ya Wanahabari pamoja na mambo mengine itasimamia kanuni za maadili ya uandishi wa habari na kuendeleza misingi bora ya maadili na nidhamu kwenye tasnia ya habari. Aidha, Baraza Huru

la Habari pamoja na mambo mengine litaweka kanuni za maadili kwa tasnia ya habari na litahimiza kufuatwa kwa misingi ya taaluma ya habari miongoni mwa wanahabari na vyombo vya habari.

**Ndugu Washiriki;**

Sheria hizi pia zinasisitiza juu ya utoaji wa habari na taarifa za Serikali kwa umma kuwa si jambo la utashi tena bali ni matakwa ya kisheria kama ilivyoainishwa katika Sheria na Kanuni zake. Ni kwa sababu hii, Maafisa Habari wa Serikali katika Wizara, Taasisi, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji ni watekelezaji wakubwa wa Sheria hizi. Mna wajibu wa kuhakikisha kwamba mnatoa taarifa mbalimbali kwa wananchi zinazohusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali lakini pia kuwa kiungo kati ya wananchi na Serikali yao.

**Ndugu Washiriki,**

Sheria ya Huduma za Habari imehuisha pia kazi zenu kwa kutamka bayana mambo mawili ambayo kwangu ni ya muhimu sana katika kuboresha majukumu yenu ya kila siku. Sheria hiyo imeainisha majukumu ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari-*MAELEZO* kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali. Aidha, Mkurugenzi huyo ambaye ninyi mnamsaidia kutekeleza majukumu yake katika maeneo mlipo, ametajwa bayana kuwa ndiye Mshauri Mkuu kwa Serikali katika mawasiliano na umma. Hivyo kwa nafasi zetu, ninyi nyote ni Wasemaji na washauri wa habari katika maeneo yenu.

**Ndugu Washiriki,**

Nafahamu wapo Maafisa Habari na Uhusiano mnaojituma katika kutekeleza majukumu yenu. Hata hivyo, kama zilivyo kada nyingine, zipo changamoto mbalimbali mnazokutana nazo katika utendaji wenu wa kazi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Kutoshirikishwa kwenye vikao vya Menejimenti ambavyo hujadili na kufanya maamuzi juu ya mipango mbalimbali na utekelezaji wake;

ii. Kutotengewa bajeti au kupewa bajeti ndogo kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Kitengo cha Habari;

iii. Kutoshirikishwa kwenye ziara ya kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara au Taasisi;

iv. Baadhi ya Maafisa Habari kuwekwa chini ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambapo majukumu yake hayapewi kipaumbele; na

v. Kutokuwa na bajeti ya inteneti na simu.

Kutokana na kuwepo kwa changamoto hizi na nyingine ambazo zinawafanya Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kushindwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu, natoa wito kwa Viongozi wa Wizara, Taasisi, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi.

Kwa kufanya hivyo, Maafisa hao wataweza kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Aidha, viongozi watambue kuwa, Afisa Habari ndiye Mshauri Mkuu katika eneo lao kuhusu masuala ya habari. Sifa kubwa ya Afisa habari ni kuwa na habari; aijue taasisi yake kwa kina; anaandaa tarifa na habari kitaalamu ili wananchi wajue nini kinaendelea na anatakiwa kuwa mbele kushauri viongozi wake kuhusu mikakati ya habari.

**Ndugu Washiriki,**

Pamoja na changamoto hizo, yapo pia malalamiko kutoka kwa baadhi ya viongozi juu ya baadhi ya Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano kushindwa kujituma na kufanya kazi kwa weledi licha ya kupata fursa mbalimbali zinazowawezesha kutekeleza majukumu yao.

Wapo maafisa wanaoshiriki kwenye vikao vya menejimenti na kujua mipango na maamuzi mbalimbali yanayotolewa na Wizara au Taasisi wanazofanyia kazi; wapo Maafisa ambao vitengo vyao vinapangiwa bajeti ya kutosha kutekeleza majukumu yao lakini wanashindwa kufanya hivyo; wapo maafisa wanaoshiriki kwenye ziara na viongozi wao lakini hawaandiki habari juu ya ziara hiyo; wapo Maafisa wanaofanya kazi chini ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kupewa mahitaji yote yanayohusu majukumu yao lakini wanashindwa kutekeleza ipasavyo majukumu hayo; wapo Maafisa ambao wana vitendea kazi maofisini, tena vya kisasa lakini hawavitumii kutangaza shughuli za wizara au taasisi zao.

Hivyo, utakapofika wakati wa kujitathimini lazima tuangalie masuala haya ili tuweze kupanga mikakati yenye tija badala ya kunyoosheana vidole baina yenu na viongozi. Ni wakati muafaka pia mkajiwekea malengo

ambayo yatatumika kupima utendaji kazi wa Maafisa habari wa Serikali. Malengo hayo yazingatie Mpango wa Taifa wa Maendeleo, Mpango Mkakati wa kila Wizara au Taasisi, Hotuba za Rais na Viongozi wa Juu pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025. Kwa Maafisa Habari na Uhusiano ambao hawatafikia malengo yaliyowekwa, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma. Hivyo, natoa rai kwenu kuhakikisha kwamba, wananchi wanahabarishwa kila mara kuhusu juhudi za Serikali katika kuwaletea maendeleo ili waendelee kuiamini na kuiunga mkono.

**Ndugu Washiriki;**

Kwa vile suala la utoaji habari ni la kitaaluma, ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa habari au taarifa tunazozitoa zinajitosheleza. Ziwe zenye ubora na maudhui yaliyozingazia ukweli, uwazi, usahihi na usawa. Natambua kuwa, pamoja na sifa hizo, dunia ya sasa inakwenda pia na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Ni wakati muafaka kwa Maafisa Habari kutumia teknolojia hii katika kusambaza habari zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali na mafanikio yake kwa wananchi. Natoa wito kwa Viongozi wa Wizara, Taasisi za Serikali pamoja Halmashauri kuhakikisha Vitengo vya Mawasiliano Serikalini vinakuwa na vitendea kazi vya kisasa kama vile kamera, lens, laptop, intaneti na vifaa vingine muhimu ili kurahisisha usambazaji wa habari zinazohusu mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yao kupitia vyombo vya habari. Ni muhimu kumuwezesha Afisa Habari kuwa na mawasiliano ya intaneti wakati wote mahali popote kwani wakati sisi Viongozi tumemaliza shuughuli zetu, wao wanakuwa

wakiendelea na jukumu la kuhakikisha wanazichakata taarifa na kuzisambaza katika vyombo mbalimbali vya habari, hivyo ni muhimu sana kuwezeshwa ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

**Ndugu Washiriki;**

Mkumbuke kuwa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 inatekeleza takwa la Kikatiba Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa mwananchi haki ya kupewa taarifa. Hivyo, kutotoa taarifa za utekelezaji wa Serikali ni kuvunja Sheria na pia Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na hayo, kutotoa taarifa za utekelezaji ni kufifisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwani inafanya kazi kubwa kuwaletea wananchi maendeleo kupitia miradi mbalimbali kama vile miradi ya maji, umeme, reli, barabara, huduma za afya, elimu na mingine mingi. Utekelezaji wote huu unapaswa kufahamika kwa wananchi ili waweze kuwa na taarifa na kuwawezesha kufanya maamuzi yatakayo rahisisha maisha yao kupitia utekelezaji huu wa Serikali.

**Ndugu Washiriki,**

Natambua kuwa vipo vyama mbalimbali vya kitaaluma vilivyoanzishwa nchini. Niwapongeze kwa kuanzisha Chama chenu cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali (TAGCO). Chama hiki ni hazina kubwa katika kuleta mageuzi na maendeleo ya kada hii Serikalini. Nawapongeza viongozi waliopo madarakani, na Wizara yangu kama msimamizi mkuu wa sekta ya habari itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa pale utakapohitajika katika kufanikisha malengo yake. Nimeelezwa kuwa katika Kikao Kazi hiki

pia kutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa TAGCO, nitumie fursa hii kuwatakia uchaguzi mzuri na wa kidemokrasia. Chagueni Viongozi watakaosaidia kuwaunganisha na kuwaletea maendeleo. Chagueni viongozi watakaojenga uhusiano mzuri na Serikali pamoja na wadau na kujenga taswira nzuri ya TAGCO mbele ya jamii.

**Ndugu Washiriki;**

Kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda niwashukuru sana Maafisa Habari kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya katika kutangaza shughuli za Seriakali. Hongereni sana na endeleeni kutimiza wajibuwenu na sisi viongozi wenu tutaendelea kuwapa ushirikiano na msaada wowote mtakaouhitaji ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi.

Aidha, niipongeze Idara ya Habari-MAELEZO pamoja na TAGCO kwa maandalizi mazuri ya Kikao Kazi hiki. Hakika mnastahili pongezi kwa kazi hii nzuri.

**Ndugu Washiriki;**

Kipekee niwapongeze na kuwashukuru wadau na wafadhili waliosaidia kwa hali na mali kufanikisha Kikao Kazi. Wadau hawa ni pamoja na TBC, Clouds Media, EFM, EATV, Kampuni ya Magazeti ya Serikali, NMB, CRDB, TPB Bank, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, NSSF, PSSSF, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, TANAPA, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, TMDA, Shirika la Bima la Taifa, WHC, TCRA, VETA, WCF, TSF,Wakala wa Huduma za Misitu, TANESCO, Tume ya Uchaguzi, Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania, TTCL, Multichoice Tanzania, VETA, TIRA,

FAIDIKA, RADIAN, eGA, DAWASA, Pharm Access Foundation, Hospitali ya Taifa Muhimbili, TIC, Ofisi ya Rais-TAMISEMI pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hakika tunawashukuru sana kwa mchango wenu.

**Ndugu Washiriki;**

Baada ya kusema haya, nitamke rasmi kuwa Kikao Kazi cha 14 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kinachofanyika hapa Mbeya sasa kimefunguliwa.

***Mungu Ibariki Afrika,***

***Mungu Ibariki Tanzania,***

***Mungu Wabariki Maafisa Habari.***

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**